



Hakika katika Jihadi kubwa ni kusema neno la uadilifu kwa kiongozi dhalimu

Imepokelewa kutoka kwa Abii Saidi Al-Khudry radhi za Allah ziwe juu yake kutoka kwa Mtume -rehema na amani ziwe juu yake- amesema: "Hakika katika Jihadi kubwa ni kusema neno la uadilifu kwa kiongozi dhalimu".

[حسن لغيره] [رواه أبو داود والترمذي وابن ماجه وأحمد]

Alibainisha Mtume rehema na amani ziwe juu yake kuwa moja ya aina kubwa ya jihadi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na yenye manufaa makubwa ni neno la uadilifu na ukweli mbele ya mtawala au mfalme dhalimu, kwa sababu ni kuifanyia kazi sheria ya kuamrisha mema na kukatiza maovu, iwe kwa maneno au maandishi au vitendo, au kitu chochote kile, ili kuleta manufaa na kuzuia maovu.

<https://sunnah.global/hadeeth/sw/show/3045>

النجاة الخيرية
ALNAJAT CHARITY

